

JE, WEWE KAMA MDAU WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA UTANUFAIKAJE NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE?

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Katika makala hii tunakusudia kuangalia mambo ambayo wewe (mdau) unatarajia kunufaika nayo kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma. Mambo hayo ni pamoja na utoaji wa maamuzi yenye haki na usawa katika ajira, nidhamu na rufaa kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18, 2007, Kanuni, Taratibu na Nyaraka mbali mbali zinazotolewa na Serikali. Katika utekelezaji wa majukumu yake Tume inashirikiana na wadau mbali mbali kama vile Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Idara zinazojitegemea, Wakala Watendaji wa Serikali, wananchi n.k. Majukumu yake ni pamoja na kumshauri Rais juu ya ujazaji wa nafasi zilizowazi, kufuatilia na kufanya tathmini kwa waajiri Serikalini ili kuona kama masuala ya ajira na nidhamu yanaendeshwa ama hayaendeshwi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu. Aidha, majukumu mengine ni pamoja na kupokea na



kushughulikia rufaa zinazokatwa na watumishi wa umma pamoja na mamlaka za nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Ndugu msomaji wadau wa Tume ya Utumishi wa Umma wanaweza kunufaika na utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia misingi ifuatayo:

- ***Kupandishwa vyeo kwa kuzingatia, haki, usawa na uwazi.***

Miongozo kuhusu utendaji wa zoezi hili imetolewa na Tume kwa Mamlaka za Ajira, na kisha kufuatiwa na ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa miongozo hiyo inatekelezwa kulingana na maelekezo ya Tume.

- ***Watumishi kuendelezwa kitaaluma.***

Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itazifuatilia Mamlaka za Ajira ili ziweke wazi mikakati, mipango na bajeti za kuwaendeleza watumishi walio chini yao.

- ***Kuwezesha upatikanaji wa watumishi wenye sifa zinazohitajika.***

Tume itatoa miongozo kuhusu vigezo vya Ajira vitakavyotumiwa na kuratibu utekelezaji wake na kusaidia kupata watumishi wenye sifa zinazohitajika pale ambapo mwenye dhamana ya kuajiri ataomba kusaidiwa. Miongozi mwa kushindwa kuwapta watumishi wanaohitajika. Miongozi mwa



Miongozo iliyotolewa na Tume ni pamoja na Mwongozo kuhusu ajira

- ***Upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi kufanyika kwa uwazi, majadiliano, haki na usawa.***

Kulingana na utaratibu mpya uliotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma juu ya upimaji wa utendaji kazi kwa mtumishi, zoezi hili kwa hivi sasa litafanyika kwa uwazi na majadiliano kati ya mtumishi na Mkuu wa kazi, tofauti na hapo awali ambapo upimaji huo ulifanywa kwa siri na Mkuu wa kazi pekee. Ili kutekeleza zoezi hilo mwajiri ataweka malengo ya kipindi husika na mtumishi ataingia mkataba wa utendaji kazi kwa kuzingatia sehemu ya majengo ambayo mwajiri amepanga kuyafikia. Mwajiri atahakikisha upatikanaji wa fedha na vitendea kazi ili mtumishi aweze kutimiza mkataba wa utendaji.

- ***Kuwepo na utaratibu ambao ni wa haraka na usio wa upendeleo.***

Kwa mujibu wa kifungu cha 62 [2] cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Tume inatakiwa kupokea, kuchambua na kutoa maamuzi ya rufaa ndani ya siku 90 baada ya kupokea vielelezo vya rufaa husika. Aidha, Tume itaratibu zoezi hili la mashtaka ya nidhamu ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za nidhamu zinashughulikia masuala hayo kwa wakati, haki na uwazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.



- ***Kuwafanya watumishi kujisikia kuwa wao ni sehemu ya mamlaka wanayoifanyia kazi.***

Kwa kuwa mwajiri amepewa Mamlaka ya kumwajiri, kumpandisha cheo na kumchukulia hatua za nidhamu, mtumishi atajiona na kujisikia kuwa yeye ni sehemu ya Mamlaka anayoifanyia kazi, badala ya utaratibu wa zamani ambapo alifanya kazi kwa Mamlaka moja na wakati huo huo akiwa anawajibika kwa Mamlaka nyingine.

Aidha, kwa kupitia Wizara husika., Tume itahakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji (Service Schemes) za makundi mbalimbali katika Utumishi wa Umma zinaandaliwa na kutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Tume ya Utumishi wa Umma inawaomba wadau wote kutoa wa ushirikiano wa hali ya juu katika utekelezaji wa majukumu yake ili kuboresha utumishi wa umma ambao ndio muhimili mkuu wa uchumi wa Nchi yetu

Iwapo una maoni au maswali tuandikie

Katibu

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

S.L.P. 9143

Dar Es Salaam

